


Khalai azungumza na mimea



-  Ursula Nafula
-  Jesse Pietersen
-  Ursula Nafula
-  2
-  Kiswahili SW



Khalai ni msichana mwenye umri wa miaka saba. Jina lake lina maana ya 'aliye mzuri' katika lugha yake ya Lubukusu.



Khalai anaamka na kuongea na mmea mchanga wa Mchungwa, "Tafadhali mti wa Mchungwa, kua mkubwa uzae machungwa mengi mabivu."



Khalai anaenda shuleni na njiani anaongea na Nyasi, "Tafadhali Nyasi, kua kijani zaidi na zaidi na wala usikauke."



Khalai anayapita Maua ya mwituni na kusema,
“Tafadhali Maua, endelea kunawiri ili niweze
kukuweka kwenye nywele zangu.”



Akiwa shuleni, Khalai anazunguumza na Mti ulioko katikati ya shule, "Tafadhali Mti, toa matawi makubwa ili tusome chini ya kivuli chako."



Khalai anazunguumza na ua unaoizingira shule yake, "Tafadhali ua, kuwa mwenye nguvu ili uzuie shule yetu kutokana na watu wabaya."



Anaporudi nyumbani alasiri, Khalai
anautembelea mti wa Mchungwa kuangalia
kama machungwa yameiva.






“Machungwa bado mabichi,” Khalai anashusha pumzi. “Nitakuona kesho, we mti wa machungwa. Labda utanipa chungwa bivu wakati huo.”



Global Storybooks

globalstorybooks.net

Khalai azungumza na mimea

-  Ursula Nafula
-  Jesse Pietersen
-  Ursula Nafula

